

HIFADHI ya Mwambezi imesheheni ndege waliohamia toka South Africa



Hifadhi ya Mwambesi iliyopo wilayani Tunduru mkoani Ruvuma licha ya kwamba haifahamiki vizuri, ina umaarufu mkubwa wa uwepo ndege maarufu waliohamia toka Hifadhi ya Taifa ya Kluger iliyopo nchini Afrika ya Kusini.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anawataja ndege hao kuwa ni aina za Rock pratincole, gloreole, white fronted sand plover na bundi anayevua samaki.

Utafiti uliofanywa katika hifadhi hiyo kati ya mwaka 2014 hadi 2015 umebaini kuwa ndege hao wamehamia katika hifadhi hiyo ambayo mazingira yake yanafanana na ya nchini Afrika ya kusini.

Hifadhi ya Mwambesi ipo umbali wa kilometra 80 toka mjini Tunduru ikiwa kando kando mwa mto Ruvuma. Licha ya kuwa na ndege hao wa ajabu, Hifadhi ya Mwambesi ina wanyama adimu wakiwemo samba, chui, tembo na wanyama wengine wengi.

Afisa Maliasili na Utalii wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe anaeleza kuwa hifadhi hiyo ilitangazwa katika gazeti la serikali kwa mara ya kwanza mwaka 1956 na kuweka chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Hifadhi hiyo ina ukubwa wa kilometra za mraba 104,052, ikiwa inapakana na mito ya Ruvuma, Msenjewe na Mitesa na kwamba eneo la mpaka na Msumbiji limechukua ukubwa wa kilometra 6.7 likiunganishwa na mto Mwambesi na Msenjewe.

Challe anabainisha zaidi kuwa Hifadhi ya Mwambesi inapakana na vijiji vya Misechela, Meamtwa, Chiungo, Amani, Nasya, Muungano, Angalia, Mwenge, Imani na Kazamoyo.



Hifadhi ya Mwambesi ina vivutio adimu vya utalii vikiwemo maporomoko ya maji ya Sunda(Sunday water falls) ambayo yapo kando kando mwa mto Ruvuma, eneo hili pia lina visiwa na fukwe ambazo zimejengwa Kambi ya utalii.

Kilima cha Mchengula na bwawa la umeme wa maji la Lisimililo ni mionganini mwa maeneo maalum ambayo yanatumiwa na wanyama kwa ajili ya kujificha na malisho.

Utalii ni mionganini mwa sekta zinazochangia mapato ya nchi na kuongeza fedha za kigeni, hivyo kipaumbele kikitolewa inaweza kufungua milango ya utalii katika mkoa wa Ruvuma.

Imeandaliwa na Albano Midelo 0784765917